

MAADHIMISHO YA KUMBUKUMBU YA SIKU YA KICHAA CHA MBWA
DUNIANI TAREHE 26 SEPTEMBER MPAKA 02 OKTOBA 2022

**KAULI MBIU: KICHAA CHA MBWA, AFYA MOJA, VIFO SIFURI (RABIES,
ONE HEALTH, ZERO DEATHS)**

1. UFUGAJI WA MBWA KWENYE JAMII YA WATANZANIA

Mbwa wamekuwa wakifugwa na binadamu tangu ustaarabu ulipoanza na wanafugwa kwa malengo mbalimbali yakiwemo ulinzi, kuchunga mifugo, uwindaji, n.k. Zaidi ya asilimia 98 ya mbwa wanaofugwa nchini ni wa asili (mongrel) na mbwa wachache ni wa kisasa ambao hufugwa zaidi maeneo ya mjini.

2. MATUNZO YA MBWA

Mbwa kama mifugo wengine wanatakiwa kupatiwa huduma zote za msingi kama chakula, maji, matibabu, malazi na kuogeshwa kwenye dawa za kuuwa wadudu. Kulingana na Sheria za Tanzania, mbwa hatakiwi kuachwa anatembea mitaani.

3. TAHADHALI ZA KUCHUKUA UNAPOFUGA MBWA

- (i) Hakikisha mbwa wako anafungiwa kwenye banda au mnyororo muda wote wa mchana. Kwa mbwa wanaotumika kwa kazi za kuchunga mifugo au kuwinda, ni vema wakawa chini ya uangalizi wa mwenye mbwa ili wasidhuru watu wengine;
- (ii) Ni vema mbwa akapata mafunzo ya msingi ili aweze kutii amri ya mwenye mbwa;
- (iii) Usimchokoze au kumpiga mbwa anayepita, anayekula au mwenye watoto, hata kama ni mpole maana anaweza kukuuma na kusabisha majereha;
- (iv) Fuata utaratibu wote wa chanjo za msingi hususan dhidi ya kichaa cha mbwa;
- (v) Mbwa anaweza kuwekwa mkanda na mnyororo ili kurahisisha kazi ya kumshika.

4. MADHARA YA KUTOFUATA TARATIBU ZA UFUGAJI BORA WA MBWA

- (i) Kung'ata na kujeruhi watu au mifugo mingine hivyo kupata kesi;
- (ii) Kusababisha hofu na kuwa tishio kwa jamii;
- (iii) Kujisaidia hovyoyote na kuchafua mazingira;
- (iv) Kueneza magonjwa kama vile kichaa cha mbwa na tegu wa mbwa;
- (v) Kusambaza wadudu nyonya kama viroboto, kupe na utitiri.

5. KICHAA CHA MBWA NI NINI?

Kichaa cha mbwa ni ugonjwa unaosababishwa na virusi vya kichaa cha mbwa na huathiri wanyama wote hususan mbwa na binadamu. Ugonjwa huu hauna tiba bali unakingwa kwa chanjo na kuzingatia ufugaji bora wa mbwa.

6. JINSI UGONJWA UNAVYOAMBUKIZA

Kichaa cha mbwa huambiza kwa njia ya kung'atwa na mbwa mwenye ugonjwa huo. Binadamu pia anaweza kuambukizwa kwa kugusa mate ya mbwa mwenye kichaa.

7. DALILI ZA UGONJWA WA KICHAA CHA MBWA KWA MBWA

- (i) Mbwa anabadilika tabia, ama kuwa mkali au mpole kuliko kawaida;
- (ii) Mnyama pori kukosa hofu yake ya kawaida kwa binadamu;
- (iii) Mbwa atashindwa kula, kukwepa maji na kupooza miguu ya nyuma;
- (iv) Mbwa hudondosha mate mengi na ulimi kuning'inia nje ya mdomo;
- (v) Kubweka mara kwa mara wakitoa mlio usio wa kawaida.

8. MAZINGIRA HATARISHI YA KUPATA UGONJWA HUU

- (i) Uwepo wa mbwa wanaozurura mitaani;
- (ii) Kufuga mbwa bila kuzingatia chanjo dhidi ya kichaa cha mbwa;
- (iii) Kukaa karibu na maeneo ya hifadhi za wanyama pori;
- (iv) Kuchokoza au kucheza na mbwa ambaye hajachanjwa dhidi ya kichaa cha mbwa.

9. NINI CHA KUFANYA KUNAPOKUWA NA TUKIO LA KUNG`ATWA NA MBWA

- (i) Mtu aliyeng'atwa na mbwa apatiwe huduma ya kwanza kwa kuosha jeraha kwa maji mengi yanayotiririka na sabuni na apelekwe hospitali;
- (ii) Ukiona mbwa amebadilika tabia, toa taarifa haraka kwa mtaalam wa mifugo;
- (iii) Mbwa aliyebadilika tabia afungiwe kwenye kibanda kwa muda wa siku kumi akipewa chakula na maji ili kuona kama atakufa.

10. JINSI YA KUZUIA KUENEA KWA UGONJWA WA KICHAA CHA MBWA

- (i) Kuzingatia njia za kuepuka kuumwa na mbwa kama vile kumchokoza au kumpiga;
- (ii) Kumfungia mbwa bandani au kwenye mnyororo muda wote wa mchana;
- (iii) Mbwa wapatiwe chanjo dhidi ya kichaa cha mbwa kila mwaka;
- (iv) Zingatia ufugaji bora wa mbwa hasa kutokuwaacha kuzurura mitaani;
- (v) Mbwa asiingie kwenye maeneo ya hifadhi za wanyamapori;
- (vi) Mbwa wote wanaoingizwa nchini sharti wawe na ushahidi wa chanjo dhidi ya kichaa cha mbwa.

11. UDHIBITI WA UGONJWA WA KICHAA CHA MBWA NCHINI

Ili kudhibiti kuenea kwa ugonjwa wa kichaa cha mbwa:

- (i) Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine imekuwa ikitoa elimu ya ufugaji bora wa mbwa;
- (ii) Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine imekuwa ikiendesha kampeni ya kuchanja mbwa nchi nzima kila mwaka;
- (iii) Serikali imetengeneza Kanuni za Chanjo na Uchanjaji ya mwaka 2020 ambazo zinalazimisha kila mfugaji kuchanja mbwa wake dhidi ya kichaa cha mbwa kila mwaka.